asuala mbalimbali inayohusu taasisi ili fikia malengo."

NIPASHE UK 7.

# Kiwanda kipya kuwa fursa sekta ya ngozi

**Na Mwandishi Wetu**

KIWANDA kipya cha ngozi ambacho uwekezaji wake umegharimu mabilioni ya fedha kilichozinduliwa na Rais John Magufuli mwishoni mwa wiki mkoani Morogoro, kitazalisha bidhaa za ngozi zenye viwango vya kimataifa.

Kadhalika, kinatajwa kusaidia kuongeza mnyororo wa thamani wa ngozi nchini kutoka kwenye machinjio hadi kwenye soko.

Kiwanda hicho ambacho awali kinajulikana kama ACE Leather Tanzania Limited, kinaendeshwa na Kampuni ya Taifa Leather Company Limited, kwa sasa ndicho kiwanda kikubwa zaidi cha kusindika ngozi barani Afrika na kinamilikiwa na Watanzania kwa asilimia 100 ambao wamefanya uwekezaji mkubwa.

Akizungumza katika mahojiano maalum baada ya uzinduzi uliofanyika kiwandani hapo kilichopo maeneo ya Kihondo, Mkurugenzi Mtendaji wa kiwanda hicho, Onorato Garavaglia, alisema Taifa Leather Company Limited imewekeza Sh. bilioni 50 za Kitanzania katika awamu ya kwanza na ya pili ya ukarabati wa kiwanda, na kwamba uwekezaji huu utawezesha bidhaa bora za kampuni kushindana kwenye ngazi ya kimataifa.

aasi-
o
0/-

Scanned with CamScanner

**Sh.50,000>> Tozo ya pango ya kibanda kwa mwezi kwa wafany**

# Serikali yatoa angalizo kwa wazalishaji chanjo za mifugo

**Na MWANDISHI WETU**, *Pwani*

KATIBU Mkuu Wizara ya Mifugo na Uvuvi (Mifugo), Profesa Elisante Ole Gabriel, ameutaka uongozi wa kiwanda cha kutengeneza chanjo cha Hester, kuhakikisha kinazalisha chanjo zenye ubora ili nchi iondokana na utegemezi wa chanjo na bidhaa nyingine za mifugo kutoka nchi za nje.

Profesa Ole Gabriel aliyasema hayo mwishoni mwa wiki iliyopita alipotembelea kiwanda hicho kilichopo Wilayani Kibaha, Mkoani Pwani kwa lengo la kuhakikisha nchi inaondokana na uagizaji wa chanjo kutoka nje.

"Tunatamani kuwa na chanjo tunazoweza kudhibiti ubora wake na tuwe na uhakika nayo. Hivyo uwepo wa kiwanda hiki utatusaidia kuzalisha chanjo hapa hapa nchini ili kukidhi mahitaji ya wafugaji wetu na Watanzania kwa ujumla," alisema.

Alisema serikali inaweka mazingira mazuri ya uwekezaji ili mahitaji ya wafugaji na wananchi yawe yanashughulikiwa ndani ya nchi.

Katibu Mkuu huyo aliwaomba wafugaji na Watanzania kuanza kujenga utamaduni wa kuthamini bidhaa za ndani na kuondokana na dhana ya kwamba bidhaa bora ni ile inayotoka nje, wakithamini vya ndani wataongeza pato la Taifa na kukuza uchumi wa nchi.

Mratibu na Mkurugenzi wa Operesheni wa kiwanda hicho, Tina Sokoine, alisema lengo lao ni kutumia wataalamu wa ndani, lakini uhaba wa wataalamu wa masuala ya sayansi wenye ujuzi hususan wa vitendo unakwamisha dhamira hiyo.

Alisema kwa sasa wana wataalamu watatu kutoka nje ya nchi ambao wamewaajiri, lakini kwa hali ilivyo wanaona watashindwa...labda tunaweza kuomba vibali vingine vya kuajiri wataalamu kutoka nje.

"Nia yetu ni kufanya kazi na Watanzania tu, lakini bado vijana wengi tunaowafanyia usahili wanakosa ujuzi hususan wa vitendo.

Tunaiomba serikali na vyuo vinavyoandaa hawa wataalamu kuhakikisha wanajikita katika elimu ya vitendo na sio nadharia peke yake ili kukidhi mahitaji ya sasa na kulinda ajira za Watanzania," alisema.

Kuhusu uzalishaji, Tina alisema wanatarajia kuzalisha chanjo ya kwanza Aprili, mwaka huu, huku akiiomba serikali kuona uwezekano wa taasisi zinazohusika na kusimamia uwekezaji kuunganishwa ziwe na lugha ya pamoja ili kumfanya mwekezaji apate huduma zote sehemu moja bila kuhangaika kama ilivyo sasa.

Scanned with CamScanner

MAJIRA UK 5.

na Taa.
ango huo
wananchi
fu kufuata
ndoa hatari
nba watu
yo ndani ya

a Wizara,
ni Shirika
NESCO),
jini (REA),
ya Petroli
akala wa
a Pamoja
Jendelezaji
TGDC),
a Mkondo
), Mamlala
za Nishati



za
a

a fedha

# Serikali kuzifutia kodi kemikali zinazotumika kuchakata ngozi

**Na Immaculate Makilika- MAELEZO**

RAIS wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Dkt. John Pombe Magufuli amesema kuwa Serikali itashughulikia na kufuta kodi inayotozwa katika kemikali zinazotumika kuondoa manyoya kwenye ngozi wakati wa uchakataji wa ngozi.

Akizungumza mwishoni mwa wiki mkoani Morogoro, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Dkt. John Pombe Magufuli wakati akifungua kiwanda cha ngozi cha Ace Leather Tanzania Limited kilichopo Kihonda mkoani Morogoro, alisema kuwa Serikali itashughulikia na kufuta tozo iliyopo katika kemikali zinazotumika kuondoa manyoya ili kuifanya ngozi iwe kwenye ubora wakati wa uchakataji ngozi.

"Kemikali zinazotumika kuondoa manyoya ili ngozi iwe kwenye ubora hii tutashughulikia kama Serikali, wizara ya Viwanda mkafanyie kazi ili hizi kemikali zinazokuja kwenye viwanda vya ngozi tu tuzifutie kodi ili waweze kuchakata ngozi zetu. Kuna ng'ombe zaidi ya milioni 34, mbuzi zaidi ya milioni 21 ngozi zote hizi, hata samaki Sangara wa Mwanza wana ngozi na zinatumika kutengenezea viatu,"alisema Rais Magufuli.

Kuhusu malighafi za ngozi kuuzwa nje ya nchi, Rais Maguguli alisema kuwa ukiwa na kiwanda hautauza malighafi nje, ukifanya hivyo maana yake umesafirisha ajira na fedha kwa watakaoenda kuchakata nje ya nchi.

"Suala la vibali kwa wanaosafirisha ngozi ghafi nje ya nchi hilo linaweza kufanyiwa kazi na Wizara ya Mifugo, mnawatoza asilimia 80, watozeni asilimia 100 ili waache kusafirisha ngozi ghafi nje ya nchi hiyo inaweza ikawa njia ya kuzuia watu wasipeleke ngozi ghafi nje kwa kuwa viwanda vipo na uwezo wa kuchakata ngozi upo,"alisema.

Aidha, Rais Magufuli alimpongeza, Rostam Aziz, Mwekezaji wa kiwanda cha Ace Leather Tanzania Limited kwa kuanzisha kiwanda hicho ambacho kitazalisha ajira 1,000 na kumtaka kuzingatia maslahi ya wafanyakazi pamoja na vifaa.

Sambamba na hilo Rais Mauguful ameitaka benki ya CRDB kuhakikisha kiwanda cha Canvas kinaanza kufanyakazi.

INAENDELEA UK. 7

Scanned with CamScanner

# Kiwanda cha ACE Leather Tanzania mkombozi sekta ya ngozi nchini

Na Halfan Diyu, Morogoro

KIWANDA kipya cha ngozi ambacho uwekezaji wake umegharimu mabilioni ya fedha kilichozinduliwa na Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Mh.John Magufuli mwishoni mwa wiki mkoani Morogoro,kitazalisha bidhaa za ngozi zenye viwango vya kimataifa sambamba na kusaidia kuongeza mnyororo wa thamani wa ngozi nchini kutoka kwenye machinjio hadi kwenye soko.

Kiwanda hicho ambacho awali kinajulikana kama ACE Leather Tanzania Limited kinaendeshwa na kampuni ya Taifa Leather Company Limited, kwa sasa ndicho kiwanda kikubwa zaidi cha kusindika ngozi barani Afrika na kinamilikiwa na watanzania kwa asilimia 100 ambao wamefanya uwekezaji mkubwa.

Akiongea katika mahojiano maalum baada ya hafla ya uzinduzi iliyofanyika kiwandani hapo kilichopo maeneo ya Kihondo mkoani Morogoro mwishoni mwa wiki, Mkurugenzi Mtendaji wa kiwanda hicho, Onorato Garavaglia alisema "Taifa Leather Company Limited imewekeza Shilingi bilioni 50 za Kitanzania katika awamu ya kwanza na ya pili ya ukarabati wa kiwanda. Uwekezaji huu utawezesha bidhaa bora za kampuni yetu kushindana kwenye ngazi ya kimataifa."

Alisema, malighafi kama ngozi kwa matumizi ya uzalishaji wa kiwanda zitanunuliwa hapa nchini Tanzania kupitia mtandao wa mawakala na wakusanyaji kote nchini. Kampuni pia itapata malighafi za ngozi kutoka nchi jirani, hususani kutoka Zambia, Malawi na Rwanda, ingawa kwa kiwango kidogo sana.

"Wafugaji wa ndani watafaidika na kiwanda hiki kwani kuna soko kubwa la usindikaji wa ngozi na ngozi za wanyama," alisema.

Akizungumzia fursa za ajira kutokana na uwekezaji huo alisema, kufikia mwisho wa mwaka 2021,Taifa Leather Company Limited itatoa ajira za moja kwa moja kwa watu 600- wakiwemo Wanawake na Walemavu pia itatoa ajira zipatazo 9,000 zisizo za moja kwa moja.

"Ifikapo mwaka 2022, kiwanda kitatoa ajira za moja kwa moja kwa watu 1,000 na vile vile kitatengeneza ajira zisizo za moja kwa moja zipatazo 15,000," aliongeza kusema.

Kuhusu kodi za Serikali alisema, pamoja na motisha zilizotolewa kufanikisha vizuri uwekezaji wake Taifa Leather Company Limited kupitia mradi wake huu italipa karibia bilioni ishirini kwa mwaka kutipia kodi za Ongezeko la Thamani (VAT), PAYE, Kodi ya Mapato pamoja na tozo nyingine kadhaa zilizopo kwa mujibu wa sheria.

Garavaglia pia alisema kuwa moja ya mpango wa kampuni ni kuzalisha bidhaa za ubora wa juu wa ngozi kwa asilimia 100 kwa ajili ya soko ndani kwa kutumia teknolojia ya kisasa.

"Kuna viashiria vinavyoonekana kuwa sekta hii iko njiani kufufuka upya ambapo watanzania wameanza kupenda kutumia na kuthamini bidhaa za ngozi halisi zinazozalishwa hapa nchini baada ya miaka mingi kulazimika kutumia bidhaa za ngozi za bei rahisi zisizo halisi (plastiki) kutoka nje ya nchi," alifafanua.

Karibu jozi milioni 50 za viatu (zenye thamani ya takribani shilingi trilioni 2.3 kwa kiwango cha dola 20 kwa jozi) zinaingizwa nchini Tanzania kila mwaka. Kuongezeka kwa uzalishaji wa ndani wa viatu vyenye ubora kwa hivyo kunaweza kuokoa fedha ya nchi nusu ya kiasi hiki yaani Tshs 1.15 Trilioni.

Scanned with CamScanner